## BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 25 Juni, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:**

Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

II. **MASWALI:**

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

275. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kuongeza ufanisi wa utendaji, Serikali iliamua kubinafsisha huduma mbali mbali zilizo chini ya taasisi zake ikiwa ni pamoja na huduma za afya, bandari, ZAWA, ZECO na Uwanja wa ndege. Hata hivyo, kuna kila dalili kuwa Serikali bado haijafanya vizuri katika kuwasimamia watendaji wanaotoa huduma hizo.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kulibinafsisha Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC).

(b) Kwa kuwa Sekta ya Elimu haikuwa ikifanya vyema, ni upi mpango wa Serikali wa kuibinafsisha Sekta ya Elimu.

(c) Je, mpango wa Serikali wa kubinafsisha huduma za maji (ZAWA) na nishati ya umeme (ZECO) umefikia wapi.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

18. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Maeneo mengi yaliyozungukwa na bahari katika nchi yetu huathiriwa na mmomonyoko wa ardhi unaokithiri katika maeneo hayo.

Je, ni mkakati gani unaofanyika kudhibiti hali hiyo.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

157. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali iliwaahidi wafanyabiashara walioko katika soko la wajasiriamali kuwapatia mikopo kwa ajili ya kujiwezesha kufanya biashara zao kwa uhakika.

(a) Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya mikopo hiyo kwa wajasiriamali hawa.

(b) Kwa kuwa, umeshatimia takriban mwaka mmoja sasa huku hali za wajasiriamali hao zikizorota kimaisha, Je, ni lini watapatiwa mikopo hiyo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

256. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Mabonde ya Kwausinga, Mwera na Pogwa yaliyomo katika jimbo la Tumbe shehia ya Chimba ni mabonde yenye sifa ya umwagiliaji.

Je, Serikali kupitia Wizara yako ina mpango gani wa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwenye mabonde hayo.

**Wizara ya Afya:**

141. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hospitali ya Kidongo Chekundu inakabiliwa na tatizo la kuwa na uzio usiorafiki, wenye kupelekea mbwa kuingia katika eneo la hospitali pamoja na watu ambao wanaweza kusababisha vitendo vya wizi.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu vipi suala hili.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuliondoa tatizo hilo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

14. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Kiembesamaki Msingi (A) na (B) zina uhaba mkubwa wa vitendea kazi sambamba na uchakavu wa majengo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto hizo za skuli ya Kiembesamaki Msingi (A) na (B).

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

277. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba, Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) limekuwa likimiliki jenereta zisizopungua tano (5) Unguja na Pemba. Hata hivyo, kutotunzwa kwa jenereta hizo kunaweza kuzisababishia uharibifu.

(a) Je, jenereta mbili za Unguja na tatu za Pemba ziko katika hali gani kwa sasa na zinatumika kwa matumizi gani.

(b) Je, jenereta tano za ZAWA zilizonunuliwa kwa jina la ZECO ziko katika hali gani na zinatumika kwa matumizi gani.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kupambana na hali ya dharura ya umeme pale endapo kutakuwa na ukosefu ama upungufu wa umeme kutoka Tanzania Bara.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

121. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la uingizaji wa magari katika miaka ya hivi karibuni, jambo ambalo limeongeza sana uhitaji wa kutengeneza namba za usajili wa vyombo hivyo vya moto. Hali hii inaleta changamoto kadhaa katika mifumo ya usajili na udhibiti wa vyombo vya moto.

(a) Je, ni mfumo na utaratibu gani wa utoaji wa namba za usajili katika vyombo vya moto hutumiwa na Serikali.

(b) Kwa wastani (average), ni kiasi gani cha mapato Serikali hupata kwa mwaka kupitia usajili wa namba za usajili za vyombo vya moto Zanzibar.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:**

Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

**Zanzibar,**
**25 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**